

BRELA

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY



BRELA BUILDING

Plot No 20, Block No. 23,
Shaban Robert Street/
Sokoine Drive junction, P.O.-
Box 9393,
Dar es Salaam,
Tel +255 (0) 22 2212800
Baruapepe: ceo@brela.go.tz,
usajili@brela.go.tz

MWONGOZO WA KUWASILISHA TAARIFA ZA MMILIKI MANUFAA

@brela_tanzania @brela_tanzania @brela_tanzania

www.brela.go.tz

1. Mmiliki Manufaa ni mtu yeyote anae miliki zaidi ya asilimia 5% ya hisa za kampuni, au ambae ana nguvu ya kufanya maamuzi au mwenye ushawishi mkubwa wa maamuzi kwenye kampuni. Mmiliki huyo anaweza kuwa anamiliki hisa moja kwa moja au kupitia kwa mtu mwingine.

2. Taratibu za kuwasilisha taarifa za mmiliki manufaa

i. Tembelea tovuti ya BRELA www.brela.go.tz, bonyeza sehemu ilioandikwa mifumo, chagua mfumo wa wammiliki manufaa, ingia kwa ajili ya kutengeneza akaunti.
ii. Pia unaweza kuwasilisha taarifa za mmiliki manufaa kwa kutembelea kiunganishi (link) https://bo.brela.go.tz/
iii. Tengeneza akaunti kwa kutumia majina kamili ya Mkurugenzi au Katibu wa kampuni, barua pepe inayotumika na nywila kisha sajili.
iv. Ujumbe utatumwa kwenye barua pepe uliyojaza kwa ajili ya kusasisha (activate) akaunti yako.
v. Tumia barua pepe na nywila uliyoweka wakati wa kutengeneza akaunti na ingia kwenye mfumo kuwasilisha taarifa za wammiliki manufaa.

3. Jinsi ya kupata asilimia za umiliki wa hisa kwa Mmiliki Manufaa. Chukua idadi ya hisa zinazomilikiwa na mwanahisa, zidisha kwa mia moja kisha gawanya kwa idadi ya hisa zote zilizogawanywa (Issued shares). Hisa ambazo hazijagawanywa kwa wanahisa hazihusiki katika ukokotoaji wa umiliki manufaa.

Mfano: Kampuni **XYZ COMPANY LIMITED** ina mtaji wa Tshs100,000 uliogawanyika katika hisa 100 na kila hisa ina thamani ya Tshs 1,000 na iwapo kampuni ina wanahisa wawili ambao ni SANDUBE mwenye hisa 40 na SEKINDU mwenye hisa 30.

Jinsi ya kutafuta asilimia za hisa anazomiliki mwanahisa itakuwa kama ifuatavyo;
Tafuta jumla ya idadi ya hisa zilizopo kwa wanahisa; Idadi ya hisa za SANDUBE (hisa 40) na SEKINDU (hisa 30). Hivyo ni hisa 40 + hisa 30 = hisa 70 (hizi ndizo hisa zilizogawanywa)

a. Asilimia za hisa anazomiliki SANDUBE ni (40 x 100) ÷ 70=**57%**
b. Asilimia za hisa anazomiliki SEKINDU ni (30 x 100) ÷ 70=**43%**

4. Iwapo Kampuni itashindwa kupata Mmiliki Manufaa mwenye 5% kutokana na muundo wa kampuni, itatakiwa kuwasilisha taarifa za Afisa Meneja Mwandamizi anayefanya maamuzi mbalimbali kwenye kampuni.

5. Wakati wa kukokotoa umiliki manufaa inawezekana kabisa baadhi ya wanahisa wasikidhi vigezo vya umiliki manufaa hivyo kusiwe na sababu ya kuwasilishwa taarifa zao. Hapa ndipo vigezo vingine kama nguvu ya kufanya maamuzi au ushawishi wa kufanya maamuzi utaangaliwa. Iwapo vyote vitakosekana, ndipo Afisa Mwandamizi anayefanya maamuzi ya kila mara kwenye Kampuni atachukuliwa kama mmiliki manufaa.

Mfano: Kampuni ina hisa 100 na wanahisa 50, hii ina maana kuwa, kwa kila mwanahisa akiwa anamiliki hisa 2 basi wote watakosa vigezo vya kuwasilishwa taarifa zao kwa kigezo cha kutokidhi asilimia 5% za hisa kwakuwa watakuwa na asilimia 2% tu kila mmoja.

6. Pia, iwapo kampuni ina hisa 100 na ina wanahisa 10 na mwanahisa mmoja akawa na hisa 90 wakati wanahisa 9 wanamiliki hisa 1 tu kila mmoja, hivyo mmiliki manufaa atakuwa ni mmoja tu mwenye hisa 90.

7. Mmiliki Manufaa anaweza kuwa wa moja kwa moja; yaani mwanahisa ambaye pia ndiye huyo huyo mmiliki manufaa au asiye wa moja kwa moja; yaani mwanahisa anaemiliki hisa kwa niaba ya mtu mwingine anayenufaika nazo.

8. Kampuni ina wajibu wa kuwasilisha taarifa kwa Msajili wa Kampuni endapo mwanahisa anaeonekana kwenye nyaraka za usajili wa kampuni na pia kwenye mfumo wa usajili mtandao (ORS) ndiye huyo huyo Mmiliki Manufaa.

Ada ya uwasilishwaji wa taarifa hizo ni Tshs. 22,000 kwa kila mmiliki manufaa na Tshs 2,500 tozo ya ucheleweshwaji kwa kila mwezi.